UQAB
Jarida la
TOLEO MAALUM
Toleo 33 - Safar 1441 H / Octoba 2019 Miladi






# Hakuna Suluhisho Kashmir Isipokua Kuandaa Jeshi la Waislamu Kuikomboa



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR

## NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 1

#KhilafahItakomboaKashmir

**629**

Kupitia mchakato wa kibiashara baina ya Waarabu na Wahindi, Uislamu ukaweza kufika katika fuo za India. Ni katika uhai wa Mtume Muhammad (saw) ndipo msikiti wa kwanza, **Cheraman Juma Masjid** ulijengwa ndani ya Kerala, India.

**711**

Waislamu walikaa kwa kudumu nchini India. Upanuzi mkubwa wa Uislamu nchini India ulifanyika wakati wa Utawala wa **Khilafah ya Ummaya**, uliokuwa na makao makuu Damascus. Mwaka 711, Utawala wa Ummaya ukamchagua kijana wa miaka 17 kutoka Ta'if kupanua Utawala wa Ummaya katika eneo la Sindh: Muhammad bin Qasim.

**714**

Sindh yote na eneo la chini la Punjab likaingizwa chini ya **dola ya Kiislamu ya Khilafah** kupitia Muhammad bin al-Qasim.

**724 - 743**

**Chini ya Khilafah ya Hisham bin Abdul Malik** maeneo ya Kashmir na Kangra yakaingizwa ndani ya Uislamu.

**1198**

**Delhi ilifanywa kuwa ndio mji mkuu wa Waislamu nchini India.** Chini ya kiongozi Mu'izz ad-Din kulipatikana serikali madhubuti. Alikuwa ni miongoni mwa watawala wakubwa wa **Utawala wa Ghurid** na anatambulika kwa kuweka msingi wa utawala wa Waislamu katika bara dogo la India.

**1526**

Babur mtawala wa kwanza wa Utawala wa Mughal akaiweka Delhi chini ya utawala wake. Akaanzisha **utawala mkubwa wa Mughal** ambao ulitawala sehemu kubwa ya India na Pakistan kwa karne mbili, wakieneza na kumakinisha Uislamu katika Asia Kusini.

**1615**

Uingereza unaanza jaribio la kuingia bara la India. **Sir Thomas Roe** aliagizwa na James I kumzuru mtawala wa Mughal **Jahangir**. Kwa mtizamo wa Uingereza mpango wao ulifaulu pakubwa.



Email: info@uqab.or.ke



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 2

#KhilafahItakomboaKashmir

**1658**

**Aurangzeb Alamgir** anakuwa Sultan na anatambulika kwa kujitolea kwa ajili ya Uislamu. Kupitia kujitolea huko, kukapelekea kuchelewesha mchakato wa kuusambaratisha **Utawala wa Mughal** kwa miongo kadhaa na huku upanuzi wa maeneo ulikuwa mkubwa wakati wa utawala wake.

**1757**

Kuanza kwa **uvamizi wa Uingereza**. Uingereza ilikuwa ikifanya biashara ndani ya India tangu 1600 lakini haikuanza kuteka sehemu kubwa za ardhi mpaka 1757 baada ya Vita vya Plassey.

**1857**

Kuanzia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, uasi ukaanza kutokea katika maeneo mengi ya bara hilo dogo dhidi ya utawala wa Uingereza na kupelekea mwaka 1857 **“Vita vya Kwanza vya Uhuru.”** Wanachuoni wakatoa fatwa kuwalazimisha Waislamu wa India wasishirikiane na Uingereza na lau hawangeweza kufanya hivyo, basi wafanye **hijrah** kutoka India.

**1919**

**Maulana Muhammad Ali Jauhar** na kakake Shaukat Ali kutoka India wakapanga kundi la Waislamu na kubuni **Harakati ya Khilafah**, muungano wa uchajimungu ambao lengo lake ni kuinusuru Khilafah kwa hali yoyote ile wawezayo.

**1924**

Kufuatia kuvunjwa kwa Khilafah mnamo 3 Machi 1924 **Muhammad Ali Jauhar** akasema, kama ilivyoripotiwa katika Gazeti la Times, “Ni vigumu kutarajia uhalisia wa athari za ‘kuvunjwa’ kwa Khilafah katika akili za Waislamu wa India. Naweza kusema kwa uhakika itakuwa ni janga kwa Uislamu na ustaarabu.” Huku Khilafah ikiwa imevunjwa, Uingereza ikaendeleza udhibiti wa India kwa kupatiliza tofauti baina ya Wahindi na Waislamu na kuchochea uadui baina ya pande mbili kwa kutumia mbinu inayojulikana ya “Kugawany na Kutawala” ili kukoloni na kuvamia ardhi.

**1938**

**Kongamano la Ligi ya Waislamu Mkoani Sindh** likafanya mkao wake wa kwanza ndani ya Karachi na kupitisha maamuzi yaliyopendekezo kwamba Ligi ya Waislamu wote wa India kuandaa mpango wa katiba ambao utapelekea Waislamu kupata uhuru wao kamili.

**1940**

Maamuzi ya kubuni makao tofauti ya Waislamu wa India yalipitishwa katika mkao wa mwaka wa Ligi ya Waislamu wote wa India ndani ya Lahore nakuwa ndio msingi wa historia ya Pakistan. Yaliungwa mkono na Uingereza na kupelekea hatimaye kugawanywa kwa India na kuwa dola mbili tofauti: Wahindu wengi – India na Waislamu wengi –Pakistan.



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 3

#KhilafahItakomboaKashmir

**1947 – "Sheria ya 1947 ya Uhuru wa India"** ikazipa maeneo mapya ya Pakistan na India uhuru kutoka kwa utawala wa Uingereza mnamo 14 na 15 Agosti 1947 mtawalia. Licha ya utawala wa Uingereza kuisha India, ushawishi wao ulibakia haswa ukawafanya Waislamu wa India kutonyanyuka tena na kudai sehemu yao katika bara hilo dogo. Imeendelea kuchochea uadui baina ya Waislamu na Wahindi na kupitisha kupitia Umoja wa Mataifa kwamba yale maeneo yaliyo na Waislamu wengi kubuni Pakistan na maeneo yaliyo na Wahindi wengi kubuni India. Lakini hawakuipeana Kashmir, eneo lilil o na Waislamu wengi kwa Pakistan na hivyo basi kuibakisha kuwa ni sehemu ya mgawanyiko, wasiwasi na mzozo.

**Agosti 1947 – Maharaja Hari Singh**, mtawala Muhindi wa eneo la Waislamu wengi la Kashmir akaliweka eneo hilo huru kwa miezi miwili. Akaweka saini kwa makubaliano ya kuwepo kwa serikali ya muda na Pakistan na India ili kumakinisha muendelezo wa majadiliano.

**Oktoba 1947 – Maharaja** akawapokonya Waislamu silaha na kuzisambaza kwa vijiji vya wenyeji Wahindi. Hili likapelekea kutokea kwa mapigano chini ya **kabila la Pashtoon** kutoka Pakistan. Maharaja akataka msaada wa kijeshi kutoka India. Katika kusitisha mapigano, India ikazindua mashambulizi ambayo yalipelekea katika mauaji makubwa ya Waislamu wa Jammu.

**26 Oktoba 1947 – Maharaja** akasaini **makubaliano ya muda** akaikabidhi Kashmir kwa India. Pakistan ilikataa makubaliano hayo na kudai kwamba makubaliano ya serikali ya muda bado yanafanya kazi.

**27 Oktoba 1947** – Wanajeshi wa **India** waingia **Kashmir** kupigana; na **vita vya kwanza** baina ya India na Pakistan vikaanza.

### 3 Novemba 1947

Waziri Mkuu wa kwanza wa India **Jawaharlal Nehru** alitangaza katika Redio Zote India, **"Tumetangaza kwamba mustakbal wa Kashmir hatimaye utaamuliwa na watu wake. Ahadi hiyo tunawapa sio tu watu wa Kashmir bali kwa dunia nzima. Hatuwezi na hatutoweza kuivunja."** Ahadi ilikuwa ni hatima ya mwisho ya Kashmir itaamuliwa kwa kura ya maoni ambapo watu wa Kashmir wataamua lau wataamua kujiunga na India au Pakistan. Lakini, ahadi hii haikutimizwa.


Email: info@uqab.or.ke



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 4

#KhilafahItakomboaKashmir

### 18 Agosti 1948

Maamuzi ya Umoja wa Mataifa (UN) yalipitishwa yakiagiza majeshi ya India na Pakistan yatoke. Majeshi ya Pakistan yalikuwa yanaikaribia Srinagar, mji mkuu wa Jammu na Pakistan na lau yangeendelea yangeliunganisha Kashmir kwa Pakistan. Lakini kutokana na makubaliano baina ya UN na India, uongozi wa mwanzo wa Pakistan ukaitisha kutolewa kwa majeshi na kupelekea Jammu na Kashmir kubakia maeneo ya mzozo.

### 1 Januari 1949


Makubaliano ya kusitisha vita chini ya Mohammed Ali Jinnah, kiongozi wa Pakistan, ambayo yalipelekea Kashmir kugawanywa mara mbili: sehemu moja ikiwa chini ya udhibiti wa Pakistan na sehemu nyingine chini ya udhibiti wa India.

### 1956

Jawaharlal Nehru, kiongozi wa India, iliamua kuiteka sehemu ya Kashmir iliyokuwa chini ya udhibiti wa jeshi la India na kuiunganisha kwa India na kupeperusha bendera ya India katika afisi za serikali. Na kulitambua eneo hilo la Kashmir kama sehemu isiyogawanyika ya India.

### 1957

Maamuzi mengine yakatolewa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa yaliyothibitisha umuhimu wa kutoa majeshi ya India kutoka Kashmir. Lakini, India ikapuuzilia mbali maamuzi hayo kwa kushirikiana na Uingereza.



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR

## NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 5&6

#KhilafahItakomboaKashmir

**1965**

Vita vya pili vikubwa baina ya India na Pakistan vikaanza, ambavyo vilipelekea majeruhi kutoka kila upande na kushuhudiwa vita vikubwa vya magari ya silaha na mizinga na vifaru vikubwa kuwahi kutokea tangu Vita vya Dunia vya II. Mzozo ulianza kutokana na Oparesheni ya Pakistan ya Gibralter ambayo ilikuwa inalenga kuyapenyeza majeshi katika eneo la Kashmir lililovamiwa na India ili kusababisha mapinduzi dhidi ya utawala wa India. Vita viliisha baada ya tangazo la Umoja wa Mataifa kusitisha vita lililopotangazwa kutokana na uingiliaji kati ya Marekani na Umoja wa Kisovieti.

**1972**

Kutokana na vita vya India na Pakistan mwaka 1971 ambavyo vilipelekea kubuniwa kwa dola ya Bangladesh, Makubaliano ya Simla yalitiwa saini kati ya Zulfiqar Ali Bhutto, Rais wa Pakistan na Indira Gandhi, Wziri Mkuu wa India. Makubaliano haya yalilenga kusitisha mzozo na mapigano baina ya nchi hizo mbili na kuleta uwiano. Yakapelekea kubuniwa kwa Msitari wa Udhibiti baina ya mataifa hayo mawili yanayodhibiti maeneo ya Kashmir.

**1984**

India ikavamia Siachen glacier. Siachen glacier ni sehemu ya juu ya vita duniani, ambapo India na Pakistan wamepigana nadra tangu 13 Aprili 1984 wakati wa Oparesheni ovu ya Meghdoot ya India.


**1988 - 1999**

Kilele cha upinzani ndani ya Kashmir dhidi ya uvamizi wa India - kinachojulikana kama Kashmir Intifada, lilitokea baada ya mzozo wa uchaguzi katika jimbo hilo. India ikatuma idadi kubwa ya kitengo cha usalama wake ndani ya Kashmir waliojumuisha wanajeshi, Usalama wa Mipaka na Hifadhi Kuu waliojumuisha idadi ya watu 750,000. Ili kuzima upinzani, India ikaweka AFSPA (Sheria ya Nguvu Maalumu za Wanajeshi) mnamo 1 Septemba 1990. Hii iliwapa wanajeshi nguvu za kushika, kutia kizuizini na kuua pasina mashtaka ili kudumisha amani pamoja na kuweka amri ya kutotoka nje na kuruhusu upekuzi wa nyumba wakati wowote. Wanajeshi wake wakashtumiwa kwa unyanyasaji wa kibinadamu dhidi ya Waislamu wa Kashmir, ikijumuisha mauaji ya kiholela, mateso, ubakaji na dhulma za kijinsia. Mpaka wa leo mauaji na unyanyasaji unaendelea pasina na watendaji kuhesabiwa.

**1999 –** Mzozo wa kisilaha ukatokea tena baina ya India na Pakistan katika Vita vya Kirgil katika Wilaya ya Kirgil ndani ya Kashmir. Lakini, Rais wa Pakistan, Nawaz Sharif akaagiza jeshi la Pakistan kujiondoa katika sehemu ya juu ya Kirgil baada ya kukombolewa na jeshi la Pakistan na Mujahideen katika vita vya kishujaa. Hili lilifuatiwa na Nawaz Sharif kufanya ziara ya Marekani na mkutano pamoja na Rais wa Amerika, Bill Clinton mnamo 04/07/1999. Kirgil ikakabidhiwa India.



Email: info@uqab.or.ke



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

## SEHEMU YA 6&7

#KhilafahItakomboaKashmir

**2003 –** Rais wa Pakistan, Pervez Musharraf akaanza kuachilia mbali haki ya Kashmir ya kura ya maoni na ukombozi kutoka India. Maendeleo haya yalikuwa ni muhimu kwa kuwa hakuna mtawala wa Pakistan aliyeweza kuzungumza moja kwa moja na India kuhusiana na suluhisho la Kashmir. Mnamo Juni 2003, akiwa amezuru Kambi ya David, Musharraf akatangaza kwamba ziara yake imepitisha ramani ya barabara ya kusuluhisha suala la Kashmir na akaongezea kwamba yuko tayari kwa makubaliano.

**2004 –** Rais Musharraf akakubali kwamba suala la Kashmir litashughulikiwa kama suala la nchi mbili baina ya Pakistan na India na litasimamiwa na Amerika. Pakistan ikiegemea mrengo wa Amerika na India ikiegemea mrengo wa Kisovieti ikapelekea kuongezeka kwa uingiliajji kati ndani ya Kashmir. Amerika ikatumia mazingira ya upinzani ndani ya Kashmiri kwa faida yake pale iliporuhusu Pakistan kuunga mkono harakati za upinzani ndani ya Kashmir ili kupatiliza fursa na kushawishi eneo hilo kwa kutegemea maslahi yake, hususan baada ya kuanguka kwa Umoja wa Kisovieti. Tangu 2004, Kashmir imejipata ikipoteza viongozi wengi wa harakati za upinzani kupitia wanamgambo wanaongozwa na India kwa kugawanya Bonde la Kashmir ili kusitisha upinzani.

**2011 –** Tume ya Haki za Binadamu ya Jimbo la Jammu na Kashmir (SHRC) imethibitisha kwamba kuna maelfu ya miili ambayo imejaa risasi na imezikwa katika makaburi ambayo hayana alama ndani ya Jammu na Kashmir. Kati ya miili 2730 iliyopatikana katika wilaya 4 kati ya wilaya 14, miili 574 ilitambulika kama iliyopotea ya wenyeji, ikienda kinyume na msisitizo wa serikali ya India inayosema kwamba makaburi yote ni ya wageni.

**2016 –** Nurhani Wani, kijana shujaa wa miaka 21 mpiganaji wa uhuru, aliuliwa kinyama kwa mikono ya wanajeshi Wahindi. Katika maandamano yaliyofuatia Waislamu 150 waliuliwa na maelfu kujeruhiwa. Zaidi ya watu 6,000 walijeruhiwa kwa kupigwa risasi za vijiwe. Zaidi ya watu 10,000 walitiwa korokoroni. Serikali ya India ikaweka amri ya kutotoka nje katika eneo iliyovamia la Kashmir, ikisababisha upungufu wa chakula na mahitaji msingi mengine.

**2017 –** Hali ya Kashmir imebakia tete; uchaguzi ulisusiwa; huduma za mtandao zikasitishwa; na jeshi la wanamgambo 20,000 la India likatumwa kujiunga na wanajeshi 500,000 wa India ambao tayari walikuwa ndani ya Kashmir. India ikaanza upya "oparesheni kubwa ya kupambana na ugaidi" dhidi ya Waislamu wa Kashmir. Uongozi wa Pakistan badala ya kuyaunganisha majeshi yake na kuikomboa Kashmir, ulifuata muongozo wa Amerika wa "kujizuia" katika Msitari wa Udhibiti na kufanyiakazi "uwiano" wa mahusiano kwa kutoa nafasi ya makubaliano mengi kwa India, kama kuidhoofisha kesi ya Kulbashan Yadhav, jasusi wa India aliyekuwa mikononi mwa jeshi la Pakistan, kuwadhibiti Mujahideen wa Kashmir walioko Pakistan na kuhudhuria Kongamano la 6 la Moyo wa Asia liliofanyika India.

**2018-**Picha ilisambazwa katika mitandao ya kijamii ikionyesha wanajeshi wa India wakiuvuta kwa miguu yake mwili wa mpiganaji wa uhuru wa Kashmiri aliyekufa. Picha hiyo ilipigwa baada ya wapiganaji watano kuuliwa katika wilaya wa Reasi eneo lililovamiwa la Kashmir. Wanajeshi wa India waliua takribani vijana Waislamu wanane kutoka maeneo ya Sopore, Kupwara na Reasi. Utawala wa Bajwa-Imran, badala ya kuchukua hatua kali dhidi ya vitendo vya kivita vya India, umeendelea kutegemea Umoja wa Mataifa isiyokuwa na nguvu na kile kinachoitwa Jamii ya Kimataifa kutatua suala la Kashmir na kulinda watu wake Waislamu. Hii ni licha ya kufeli kwa wazi kwa Umoja wa Mataifa ndani ya zaidi ya miongo 7 katika kutimiza ahadi yake kwa watu wa Pakistan na Kashmir.



# KALENDA YA MATUKIO YA HISTORIA YA KASHMIR NA UVAMIZI WAKE KUTOKA KWA INDIA

#KhilafahItakomboaKashmir

## SEHEMU YA 8

**14 - 2 - 2019**

Maafisa wa usalama 40 wa Hifadhi Kuu ya Jeshi la Polisi wa India waliuliwa katika shambulizi walipokuwa wanasafiri katika Barabara ya Kitaifa ya Jammu Srinagar katika wilaya ya Pulwama eneo la Kashmir. Waliodaiwa kutekeleza shambulizi hilo ni kundi la Pakistan la Jaish-e-Mohammed. Serikali ya Pakistan ilikashifu vikali ulipuaji huo na kusema kwamba iko tayari kuisaidia India katika kuwachukulia hatua kile walichokiita ‘kundi la kigaidi’ na kuviita vitendo hivyo vya upinzani dhidi ya uvamizi wa India katika Kashmir kama “ugaidi.” .

**MACHI 2019**

Mwanajeshi wa Angani kamanda Abhinandan Varthaman, alishikwa na wanajeshi wa Pakistan pale ambapo ndege yake ya kivita ilipoangushwa kwa kuingia anga ya Pakistan, alirudishwa India kwa agizo la Waziri Mkuu wa Pakistan Imran Khan kama “ishara ya amani” ili kupunguza kuzidi kwa mizozo baina ya nchi hizo mbili. Naye Waziri Mkuu wa India Narendra Modi akarudisha mkono siku hiyo hiyo, kwa kumimina risasi katika upande wa Pakistan wa Msitari wa Udhibiti kutoka kwa wanajeshi wa India ambao waliwaua wanajeshi wawili wa Pakistan. Hilo likafuatiwa na siku ifuatayo kwa kurudishwa kwa mwili wa Shakir Ullah kwa familia yake na mamlaka ya India, alikuwa ni mfungwa Mpakistan ambaye alipigwa mawe mpaka kufariki ndani ya jela ya India katika kulipiza kisasi shambulizi la Pulwama. Mwili wake ulipeanwa katika mpaka wa Wagah baina ya Pakistan na India sehemu hiyo hiyo ambayo Kamanda wa India Varthaman alirudishwa katika mikono ya India siku moja kabla.

**MEI 2019**

Imran Khan kwa furaha akatuma ujumbe katika mtandao wa Twitter kwamba “Nampongeza Waziri Mkuu Modi kwa ushindi katika uchaguzi wa BJP na washirika wake. Nina matumaini ya kushirikiana naye katika amani, maendeleo na ustawi katika Asia Kusini.” Imran anatafuta amani kutoka kwa Modi, ambaye alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Gujarat wakati wa mauaji ya halaiki ya Waislamu yaliyofanyika mwaka 2002. Alimpongeza Modi, ambaye kama Waziri Mkuu alitumia risasi za mawe kuwatia upofu na kuwakandamiza Waislamu wa eneo lililovamiwa la Kashmir. Anamatumaini ya ustawi kupitia Modi, ambaye alikiuka anga ya Pakistan na kudumisha ufyetuaji risasi katika Msitari wa Udhibiti. Na anatarajia maendeleo kutoka kwa Modi ambaye kwa ujasiri alitangaza mnamo 8 Aprili 2019 kwamba atafutilia mbali hadhi maalum ya kikatiba ya eneo lililovamiwa na India la Kashmir na kulifanya kuwa sehemu ya India lau atarudi mamlakani.

**5 Agosti 2019**

India imefutilia mbali uhuru maalum wa Kashmir kupitia agizo la rais lililopitishwa haraka huku ikituma wanajeshi 35,000 wa ziada katika eneo hilo, imekata mawasiliano ya wenyeji, imewatia korokoroni maelfu na kuweka amri ya kutotoka nje kwa Waislamu wa Kashmir. Hatua yake hiyo ya kivita ni jaribio la kuliteka eneo lililovamiwa la Kashmir kuwa India kwa kufutilia mbali Kipengee 35-A na 370 cha Katiba yake ambayo inalenga kutimiza ruwaza ya msimamo mkali wa kitaifa ya Modi dhidi ya Kashmir: ili kufungua mlango kwa Wahindi waweze kuishi ndani ya Kashmir na kubadilisha mpangilio wa idadi ya watu ndani ya eneo hilo la Kashmiri lenye Waislamu wengi ili idadi ya Wahindi iwe kubwa na kuweza kudhibiti Waislamu na Uislamu ndani ya eneo hilo.
Kwa miongo 3 iliyopita pekee, inakadiriwa kwamba Waislamu 100,000 ndani ya Kashmir wameuliwa na ilhali maelfu wameteswa, wamefungwa na kupotezwa na mamia ya vijana na watoto Waislamu wametiwa upofu au nusu upofu kwa kupigwa risasi za mawe na wanajeshi wa India wakati wa maandamano dhidi ya wavamizi wao. Kando na hayo, maelfu ya wanawake Waislamu ndani ya Kashmiri wamebakwa au kunajisiwa na wanajeshi wa India ikijumuisha kubakwa na magenge. Ukandamizaji na Uhayawani unaendelea.



Email: info@uqab.or.ke